

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

E-mail: info@ewura.go.tz

Website: <http://www.ewura.go.tz>

TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu (Karatu WSSA) (“Mwombaji”) kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Karatu. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Mwombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:

1: Jina na Anuani:
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu, S.L.P 376, Karatu - Arusha, Tanzania.
2: Maelezo ya Leseni:
Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Karatu.
3: Chanzo cha Maji na Miundombinu
Chanzo cha maji kinachotegemewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu ni Kisima cha Bwawani chenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 720 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji, inajumuisha, tanki moja (1) lenye mita za ujazo 225 na kituo kimoja (1) cha kusukuma maji (pumping station) . Vilevile, muombaji ana mtandao wa majisafi; wenye urefu wa kilomita 2.9 kwa bomba kuu la kusafirisha maji, kilomita 13.3 kwa bomba kuu la kusambaza maji, kilomita 2.3 kwa mabomba ya maunganisho ya wateja yaliyotengenezwa kwa malighafi mbalimbali (GS, HDPE na PVC), kiwango tofauti (PN10 na PN 16) na vipenyo tofauti tofauti (DN25mm mpaka DN150mm) na vituo 14 vya kuchotea maji. Aidha, muombaji hana mfumo wa kukusanya wala mitambo ya kusafisha majitaka.
4: Umiliki
Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu yeyote mwenye kukusudia kuwasilisha maoni au pingamizi juu ya maombi tajwa hapo afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi hayo zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi ya maandishi kwa anuani iliyooneshwa hapa chini:

**Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,**